



22100299



International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1
SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1
SUAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1

Thursday 13 May 2010 (afternoon)

Jeudi 13 mai 2010 (après-midi)

Jueves 13 de mayo de 2010 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.

Toa maoni yako juu ya **moja** ya tungo zifwatazo.

1.

“Kweli mji huu ni wa ajabu,” alisema Dunia huku akivuka barabara. Gari lilifunga breki ghafla miguuni mwa Dunia, ikasikika sauti kali pale magurudumu yalipochuana na lami, moshi ukapaa. Dunia alibaki kulizuia gari kwa mkono; butaa lilimpiga, mwili ukamtetemeka. Dereva alitoka garini mbio hadi alikosimama Dunia, akamshika ukosi wa shati, akamtikisa kama 5 upepo utikisavyo jani mtini. Alikuwa tayari kumnyaka makofi Dunia lakini alijikanya akiju huo hautakuwa ubinadamu hata kidogo. Hakuna mtu aliyezi kufa ila huwa ni ajali na ajali haina kinga. Alimuonya na kumtaka Dunia awe mwangalifu barabarani kisha akajipakia garini mwake akang’oa na kuondoka.

Dunia moyo ulimdunda, kijasho chembamba kikamatika, akasimama tutwe katikati ya 10 barabara kama aliyepigiliwa misumari.

“Nina bahati kama ya mtende. Ee mwenyezi Mungu, nisaidie na kuniongoza,” Dunia alijisemea na kuomba.

“Ondoka hapo basi! Njoo huku! Utakufa bure hapo! Ee! Wewe kweli u mgeni. Watoka wapi kwani?” Alisikia watu wakimpiga kelele huko magari mengine yakimpiga honi, 15 ndipo bumbuazi zilipomwishia, akavuka barabara, mkoba wake wa nguo mkononi, akatokomea hajui aendako. Baadhi ya watu walimshindikiza kwa macho huku wakivitikisha vichwa vyao kwa huruma na masikitiko.

Dunia alipatwa na wasiwasi. *Labda alifanya makosa kuyapinga mashauri ya wazee siku ile ya hadhara kule kwao.* Mji wa mwambao ulimtishia, mambo yakamkalia upande. Uamuzi wake 20 kuja kuishi mjini Mwambao ulilingia hatihati, akajiuliza iwapo ulikuwa uamuzi wa busara au la. Ghafla alijipata amevurugika akili, mbele kwatisha kwenda nyuma hakurundiki.

“Aa! Sina budi kwenda mbele, ima fa ima!” Alijipa moyo. Njaa ilimshika.

Aliingia ndani ya mkahawa karibu naye. Unadhifu mkahawani humo ulimvutia. Hata ndani ya majumba mengi huko kwao Kibaoni hamkuufikia unadhifu wa mkahawa huu. Kuta ziliremba 25 vigae vya maru maru, sakafu ikapakwa rangi nyekundu. Madirisha ya vioo yalifungua pazia za hariri. Viti vya kulalai, vya matakio manene, vilipangwa mduara wa meza ili wateja wakalie. Watumishi waliovaa bwelasuti za rangi nyeupe waliwahudumia wateja. Aliletewa kadi yenyе majina ya vyakula na bei zake. Aliagiza ugali kwa matumbo ya ng’ombe. Punde kidogo chakula 30 kiliandikwa mbele ya Dunia, akaenda akafungua mfereji wa maji akanawa mikono ndani ya bakuli pana shaba lililotundikwa ukutani. Aliufuata utaratibu waliokuwa wakifuata wateja wengine. Alirudi mezani, akala akashiba, akanawa tena mikono. Alitoa shilingi thamanini mfukoni akaenda kwa keshia akalipa na kutoka.

Alizurura hapa na pale, akaondoka huku akasimama kule, akaondoka kule akasimama huku, hadi juu likatua, magharibi ikaingia. Giza lilipoenea vizuri na hewa kuwa baridi, anga ilimemetuka 35 taa za umeme za kila rangi, nyingi kama nyota. Dunia alijua ni lazima atafute mahali pa kulala. Katika tembeatembea za mchana kutwa, aliwahi kuyaona majumba mengi ya ghorofa, ya kukondisha upate malazi. Hapo aliposimama, usiku huo, moja kati ya majumba ya malazi lilimkabili, maandishi makubwa kwenye mimu ya juu ya mlango yalisomeka: KODISHA ULALE. Alikwenda mlangoni akavipanda vidaraja hadi juu sebuleni. Alimpata bwana mmoja ameketi 40 nyuma ya meza.

Alilipa pesa za nyumba, akaonyeswa chumba cha kulala. Kitanda kikubwa cha kanzu kilitandikwa godoro pana la sifongo na mito miwili minene ya sufi. Alionyeshwa msalani. Wakati ulitimu saa tatu ya usiku na macho ya Dunia yalianza kumuasha kwa usingizi na mwili kupata maumivu mwendo wa mchana kutwa. Dunia alivua nguo akazitumbukiza 45 mkobani mwake, pamoja na pesa, akafunga taulo akenda msalani, alimojifungia ndani. Aliivua taulo, akaitundika kwenye kulabu, ukutani. Aling'ang'ana hadi akalifungua bomba la maji kisha akasimama chini ya bomba hilo lililominika maji, kama mvua, kwenye kawa lake pana la tundu nyingi ndogondogo. Alijipaka sabuni kisha akajisuza hadi akatakata. Kwisha hilo, alijifunga taulo akarudi chumbani mwake akalala. Alibumburuka usingizini 50 kulipokucha akapiga miayo na kujinyongoa. Polepole aliinuka kitandani, akauendea mkoba wake akautoa mswaki akaenda msalani kusugua meno. Alirudi chumbani akavaa nguo na kujichana nywele kisha akaufunga mlango wa chumba. Aliteremka vidaraja hadi njie akaenda mkahawani kustaftahi.

Lamin H Omar, *Dunia Mashaka Makuu* (2004)

- Tambua maudhui makuu na uonyeshe yanavyokuzwa kwenye kifungu hiki.
- Mazingira yanachorwa kivipi na yana umuhimu gani katika kifungu hiki?
- Ni sifa zipi zinazojitokeza katika kifungu hiki na zinaendelezwa kwa njia gani?
- Mwandishi amefaulu au kutofaulu katika matumizi ya lugha kwa njia gani?

2.

Mali

Kupenda mno ukwasi, naona nitapotea,
 mali ina wasiwasi, sikai nikatulia,
 mali huzua maasi, mtu yakampotoa.

- 5 Mali ni njema hidaya, hili kweli nalijua,
 sura yangu iwe mbaya, watu wataisifia,
 lakini naona haya, sifa hii kupokea.

Mali ni nzuri hidaya, tena ninakariria,
 lakini ina hekaya, ngumu kuizingatia,
 hususa huwa kayaya, dunia kuizamia.

- 10 Mali pale niko nayo, wengi wananiinamia,
 bali nikitokwa nayo, rafiki wanikimbia,
 na nipigapo miayo, pembedi wanizomea.

- 15 Mwenye mali huzuzuka, kheri akaziambaa,
 na heshi kubabaika, kushukushuku jamaa,
 na huko kafilisika, akuhofu kila saa.

Umesikia karuni, mali ilimzuzua,
 mali ilimfitini, dongo likamfukia,
 ni khatari yamkini, kwa as-habu rupia.

- 20 Maadui wa mkwasi, ni wengi kupindukia,
 rafikize si rahisi, ghalibu humdowea,
 wamchomoe fulusi, kisha wamtete pia.

Kheri nikidhiwa haja, shida zikinifikia,
 nile kadiri ya haja, na nione njaa pia,
 na niipate faraja, dhiki zikinitokea.

- 25 Ee mola wangu Bwana, Jalla wa ala Jalia,
 ufukara maulana, nakuomba nepushia,
 nipe riziki mwanana, haja kunitosheleza.

- 30 Ukinipa utajiri, nipe na elimu pia,
 mali zangu niajiri, ziwafalie insia,
 nikushukuru Qahari, vile kunifadhalia.

Kitula King'ei na Amata Kemoli, *Taaluma ta ushairi* (2001)

- Mtunzi wa shairi hili anatoa kauli zipi kuhusu mali?
 - Uteuzi wa maneno na lugha unasadida kwa njia gani upitishaji wa ujumbe?
 - Jadili kuhusu muundo wa shairi hili.
 - Tathmini jinsi mwandishi anavyojimudu katika kuitisha ujumbe, na uonyeshe jinsi unavyofikia uamuzi huo.
-